SHULE YA SEKONDARI MATANDA,
S.L.P 75,
KILWA – MASOKO.
MOBILE: ……………………..
………/………/……………

Kumb. Na. MATSS/ADM/21

Jina la mwanafunzi: ……………………………………………………..
S/M ……………………………………………………..
S.L.P ………………………..
**KILWA MASOKO.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATANDA WILAYA YA KILWA MKOA WA LINDI KWA MWAKA 20……**

## 1.0 Utangulizi

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka …………….., shule ya sekondari Matanda ipo umbali wa Kilometa 120 Kusini mwa mji wa Kilwa – Masoko. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ………./……../………….. na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ……../………./………. na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……../………./………… ndani ya siku saba.

## 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

### 2.1.Sare za shule.

**(a) Wavulana sare zao ni :-**

i. Suruali mbili za rangi ya dark blue.
ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (vyenye mikanda) na visiwe na visigino virefu.
iv. Soksi ndefu jozi mbili nyeupe (zisizo za mistari)

(b) **Wasichana sare zao ni**:-

i. Sketi mbili rangi ya blue bahari (kitambaa kizito)
ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (vyenye mikanda)
iv. Hijabu nyeupe.

Sare hizi zitatumiwa na mwanafunzi muda wote awapo darasani (wakati wa vipindi vya darasani) na mishono hii kwa wavulana na wasichana inatakiwa iwe ya heshima ya heshima kwa jamii zisiwe za kubana na zisiwe fupi.

### 2.2. Sare zingine za shule.

**(a) Wavulana sare zao ni:-**

i. Suruali mbili za rangi ya kaki.
ii. T-Shirt mbili rangi ya kijivu.

(b) Wasichana sare zao ni:-

i. Sketi mbili rangi ya kijani na shamba dress moja rangi ya kijani.
ii. T-Shirt mbili rangi ya kijivu.

***NB. T- Shirt rangi ya kijivu zinapatikana hapa shuleni.***

Sare hizizitaatumiwa na mwanafunzi muda wote awapo nje ya darasa (wakati wa shughuli za jioni). Mwanafunzi hatoruhusiwa kuwa na mavazi mengine zaidi ya hizo sare zilizotajwa hapo juu.

**2.3**. Kila mwanafunzi anatakiwa awe na nguo za michezo ikiwa ni T-Shirt moja rangi ya blue na Tracksuit moja rangi ya blue pamoja na raba kwa jinsia zote ambazo zitatumika wakati wa michezo.

***N.B. T-Shirt ya michezo na Tracksuit zitapatikana hapa shuleni.***

**2.4.** Daftari kubwa zisizopungua kumi (10), kalamu za wino, mkebe wa hesabu na Kamusi ya kiingereza.

***N.B. Kamusi zitapatikana hapa shuleni.***

**2.5.** Faili kwa ajili ya kutunzia mitihani ya masomo mbalimbali.

**2.6**. Daftari ndogo za size ya kati kwa ajili ya homework zisizopungua tisa (10).

**2.7.** Daftari ndogo za size ya kati kwa ajili ya weekly Test zisizopungua (10).

**2.8.** Mavazi yatakayotumika kwa ajili ya kuswalia Ijumaa ni Hijabu ndefu/juba jeupe kwa wasichana na kanzu/nusu kanzu kwa wavulana.

**2.9.** Mahitaji kwa ajili ya watakaokaa hosteli ni:-

a) Sanduku/Tranka na kufuri lake kwa ajili ya kutunzia nguo na vifaa vingine muhimu.
b) Godoro kwa ajili ya malazi.
c) Chakula atakachotoka nacho nyumbani.
d) Ndoo kwa ajili ya kuchotea na kuhifadhia maji.
   Vifaa hivi vitakaguliwa kabla ya mwanafunzi kuingia hosteli na asiyekamilisha hivyo hatapokelewa.

**3.0.** Wanafunzi wote watatakiwa kuja na vifaa muhimu kwa ajili ya shighuli za hapa shuleni kama vile:-

I. Jembe lenye mpini mmoja
II. Panga
III. Fyekeo
IV. Fagio la chelewa lenye mti

**4.0. Sheria na kanuni muhimu za shule ni:-**

A. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
C. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (evening preparation)
D. Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
E. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
F. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
G. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
H. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
I. Kutunza mali ya umma.

**4.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

A. Wizi
B. Uasharati na ushoga
C. Ubakaji
D. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
E. Kupigana au kupiga
F. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule na umma
G. Kudharau bendera ya taifa
H. Kuwa mjamzito au kupata mimba
I. Kuoa au kuolewa
J. Kutoa mimba
K. Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kwa kuvuruga amani na usalama wa shuleau watu
L. Kukataa adhabu kwa makusudi
M. Kuwa na simu ya mkononi

**5.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na mwanafunzi.**

A. Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
B. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayokatolewa na shule.
C. Fomu ya uthibitisho wa mwanafunzi kukubali na kutii sheria, kanuni na taratibu za shule.

**6.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatelekeza Kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**……………………………………..**

**RAJABU M. MBINGA**
**MKUU WA SHULE**

## 7.0. FOMU YA UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI WA KUKUBALI NA KUTII SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZINGINE ZA SHULE.

Mimi mwanafunzi (Jina kamili) ………………………………………………………………..................
Nimezisoma sheria, kanuni na taratibu pamoja na mwenendo bora wa shule kwa umakini na kuzielewa. Nakubali kuzitii na kuzitekeleza zote kama zilivyo.

Sahihi ya mwanafunzi:………………………………………….. Tarehe: …………………………………

## 8.0. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

Mimi…………………………………………………………………….. ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi huyu nimezisoma na kuzielewa kanuni, taratibu na sheria pamoja na maelekezo na mwenendo bora wa shule na kuzikubali kama zilivyo na nipo tayari kushirikiana na shule katika kuzitekeleza kanuni na taratibu hizo na ninaahidi kumpatia vifaa na mahitaji mengine muhimu kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule na ninathibitisha kwamba ndugu na jamaa nimewajaza kwenye fomu ya utambulisho iliyoambatanishwa na fomu hii.

Sahihi ya mzazi/mlezi (mdhamini 1) ……………………………………..
Tarehe …………………………. Namba za simu …………………………….

Sahihi ya mzazi/mlezi (mdhamini 2) ……………………………………..
Tarehe ………………………. . Namba za simu ……………………….…..

**NB.** Ndugu ambaye hakutambulishwa hatatambuliwa na uongozi wa shule pindi anapohitajika mzazi/mlezi kwa masuala ya kinidhamu.